**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**
**BODI YA USIMAMIZI WA STAKABADHI ZA GHALA**

## TANGAZO KWA UMMA

## MAFUNZO KWA MENEJA DHAMANA *(COLLATERAL MANAGER)*, MWEKA MALI *(DEPOSITOR)* NA WAFANYAKAZI WANAOHUDUMU KWENYE GHALA

Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) ni Taasisi chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara iliyoundwa kwa **Sheria ya Stakabadhi za Ghala Sura 339.** Bodi pamoja na mambo mengine imepewa jukumu la kutoa leseni ya Meneja Dhamana kama Kifungu cha 5(b) kinavyobainisha.

Bodi inapenda kuutaarifu umma, hususani Meneja Dhamana walio na leseni pamoja na wale wanaotarajia kuwa na leseni, kuwa itaendesha **mafunzo maalumu kwa Meneja Dhamana *(Collateral Manager)*, Mweka Mali *(Depositor)* na Wafanyakazi** watakaohudumu kwenye ghala mbalimbali kuelekea **msimu wa 2026/2027 wa mauzo ya zao la Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta na Choroko** kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

Lengo la mafunzo haya ni kuwaongezea washiriki uelewa kuhusu Mfumo wa Stakabadhi za Ghala, mahitaji ya uzingatiaji wa kanuni na sheria, usimamizi wa hatari, viwango vya uendeshaji pamoja na mbinu bora za usimamizi wa bidhaa.

Mafunzo haya yanatarajiwa kufanyika **Mkoani Mwanza tarehe 26 hadi 30 Januari 2026.** Gharama za mafunzo ni **Shilingi Laki Saba na Elfu Hamsini Tu (Sh. 750,000).** Gharama hii imejumuisha chakula (asubuhi na mchana), shajala pamoja na vyeti kwa watakaofaulu mtihani wa Bodi.

Washiriki wenye nia wanatakiwa kujisajili pamoja na kufanya malipo kabla ya **tarehe 21 Januari 2026.**

Kwa usajili, kupata bili ya malipo *(control number)* na maelezo zaidi, wasiliana na **Bi. Yasira Amri** kwa simu namba **0754 897 780** au barua pepe **yasira.amri@wrrb.go.tz** au **Bw. Omary Mafita** kwa simu namba **0756 630 180** au barua pepe **omary.mafita@wrrb.go.tz.**

***NB:*** *Washiriki wanaombwa kuja na kompyuta mpakato (laptop) kwa ajili ya kuwezesha mafunzo ya mifumo ya tehama ya Bodi.*

Imetolewa na;

**MKURUGENZI MTENDAJI**
**13 JANUARI 2026**